

**Mr. Munyasia:** Since we did not know who was speaking at the time when the House was adjourned, we did not stand up because we first wanted to know who was speaking at that time.

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** No!

**Mr. Munyasia:** Yes!

**Mr. Speaker:** From my list, I see that it was Mr. ole Tipis who was contributing when the House was adjourned, and he is not present now.

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** On a point of order, Mr. Speaker, Sir. Hon. Members should be aware that if the person who spoke last is not here, they should automatically stand to speak. But since there was nobody who stood to speak, and you said, "Since there is no hon. Member wishing to speak . . .", we should go ahead so that hon. Members can learn a bit of a lesson.

**Mr. Speaker:** No, I think their request is quite genuine. Mr. Munyasia.

**Mr. Munyasia:** Ahsante sana, Bw. Spika, kwa kuni-patia nafasi hii. Ni lazima Mbunge wa Butere afahamu kwamba ni lazima atupatie heshima vile tulivyompatia wakati alipokuwa akiongea.

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** Niwape heshima?

**Mr. Munyasia:** Ndio!

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** On a point of order, Sir. Nimekupa heshima uweze kukaa chini!

**Mr. Munyasia:** Bw. Spika, Hoja hii ya maongozi ya taifa juu ya chakula ni muhimu sana. Tukiangalia au kusafiri katika nchi nyingine, tutaona kwamba kuna nchi nyingine ndogo ambako mvua inayonyesha ni chache lakini wana mipango kamili ya kujipatia chakula. Kwa mfano, hivi majuzi tulipokuwa tukitoka katika visiwa vya Philippines, tulipita juu ya Bangkok na tukaona vile watu wa nchi hiyo wametega maji ya mvua na kuyatumia kwa kunyunyizia mashambani na vile nchi hiyo yote inavyojaa mchale. Nafikiri ni juu ya Waziri wa Kilimo akishirikiana na Wizara ya Ustawi wa Maji, washauriane na kufanya mpango kamili ili kuona kwamba maji yote, ambayo ni ya Mungu—maji ni ya Mungu na si ya mtu yeyote—yanayotoka mbinguni yanazuiwa yasiende katika Bahari Hindi.

Bw. Spika, nchi hii ya Kenya imefanikiwa sana, na hasa katika pande za Ukambani. Mungu aliumba kila mahali kulingana na matakwa yake. Hivi majuzi kulikuwa kunasemekana kuwa kulikuwa na njaa katika sehemu ya Ukambani; hayo si matakwa ya Wakamba, lakini ni vile Mungu alivyoiumba sehemu hiyo, na tutakaa huko huko kukiwa namna hiyo. Katika season iliyopita, mvua ilinyesha na sasa ukienda kule Ukambani, utaona kila mahali ni green na watu wana chakula. Lakini hakuna mipango ya kutoa chakula. Tunaweza kusema kuwa katika sehemu ya Ukambani kote kuna mito na vijito, lakini maji huko hayatulii; mvua inaponyesha maji yanakwenda moja kwa moja mpaka baharini. Ni kwa nini Serikali haiwezi kufikiria na kuona kwamba mpango kamili unafanywa, hata

ikiwa ni kwenda kukopa pesa kutoka nchi za ng'ambo, kwa mipango ya maji, ili mito hii yote ipate kujengewa reservoirs, ili wakati mvua inaponyesha maji yawe hayawezi kwenda baharini yote? Hii ndio sababu ninasema hatuna mipango kamili.

Kesho Mtukufu Rais atakwenda kufungua project moja kule pande za Masinga. Eneo hilo lilikuwa kavu kabisa na mto huo ulikuwa mkavu kabisa. Wale wata-kaokwenda kule wakirudi hapa watakuja kusema maneno mengine kabisa kwa sababu ukienda kule, kume-kuwa na ziwa moja ajabu sana la kipekee katika Afrika Mashariki; hakuna ziwa lingine kama hilo katika Afrika Mashariki. Huo mto ulikuwa mkavu sana na hata maji yake yalikuwa hayaonekani na watu wa upande huo walikuwa wakiumia sana. Lakini sasa maji yamezuiwa na yamejazana umbali wa karibu kilomita 52 mpaka karibu Embu. Basi ikiwa tunataka kumaliza shida za njaa, ni lazima tukuze chakula kingi ili kuona kwamba hatutakabiliwa na njaa tena. Kufanya hivyo, ni lazima tuseme, kwa mfano, "Katika budget ya Kenya mwaka huu tutakuwa na kiasi fulani cha kustawisha maji peke yake", kuliko kusema tu, "Oh, hakuna pesa", au "tunaangalia vile maji yatakvoyopatikana", na mambo kama hayo.

Bw. Spika, Wazungu wanapatiana conditions kutoka kwao na kusema, "Mkinita huko kwenu, nitawapatia \$200 million", halafu anatumwa na kuja hapa. Akija hapa atakuwa anafuata zile pesa na aanze kusema, kwa mfano, "Ni lazima twende mahali kwenye mto ili tuchore na kufanya mambo mengine", na wakati huo huo anaendelea kutumia zile pesa. Wakati huo huo, ukiangalia katika estimates, utaona kwamba nchi za ng'ambo, Marekani ikiweko, wamepatia nchi ya Kenya milioni nyingi za pesa na kiasi cha K.Sh. 200 milioni kimekwenda Ukambani. Ni ajabu kukueleza, Bw. Spika, kwamba Wilaya ya Machakos ilipatiwa kiasi cha K.Sh. 200 milioni ili kustawisha maji.

[Mr. Speaker left the Chair]

[Mr. Deputy Speaker took the Chair]

Tangu tusome habari ya pesa hizo, sasa ni miaka minne iliyopita na ukienda kule Machakos, lazima utajiuliza, "Je, zile K.Sh. 200 milioni zilizopeanwa ili kustawisha maji katika wilaya hii ziko wapi au zime-enda wapi?" Kwa sababu hakuna chochote ambacho kimefanywa huko. Wale watu waliopana pesa hizo ndio waliotoa condition kuhakikisha kwamba wame-fuata pesa hizo na kuzitumia, halafu waandike katika makaratasi kuwa "tulisaidia watu wa nchi ya Kenya". Yaani ni lazima kuwe na mchoro ambao utagharimu Sh. 100,000 na watu watakaokuja kufanya kazi ni lazima wapatiwe malazi yatakayogharimu karibu K.Sh. 3,000 kwa siku. Watu hawa wanakaa mwaka mmoja na pesa hizo zinakwisha. Machakos ilipatiwa Sh. 200 milioni lakini hakuna maji; hiyo bado ni sehemu kavu, na hakuna chochote.

Kwa hivyo, hii ndiyo sababu ninasema kwamba mipango tuliyo nayo siku hizi ni mibaya. Ikiwa watu wanataka kukopesha nchi yetu pesa, ni lazima tuone kwamba hawafuati pesa hizo na kuja kuzifanyia kazi.

**[Mr. Munyasia]**

Bw. Naibu Spika, ningemwomba Bw. Charles Rubia amwachilie mbali Makamu-Rais na Waziri wa Fedha ili aweze kusikia yale mambo ninayoyasema. Hili ni jambo la muhimu sana.

**The Minister for Urban Development and Housing (Mr. Rubia):** On a point of order. Bw. Naibu Spika, ni haki kwa Mhe. Mbunge kunitaka nimwachilie Makamu-Rais na Waziri wa Fedha na hali hawataji wale Waheshimiwa Wabunge wengine?

**Mr. Munyasia:** Ni haki, Bw. Naibu Spika, kwa sababu ninaongea juu ya fedha na ni Makamu-Rais na Waziri wa Fedha anayetayarisha mipango ya fedha. Hili ni jambo la maana sana. Sababu iliyonifanya niseme ni heri amwachilie, au ampatie nafasi Makamu-Rais na Waziri wa Fedha ni kwamba—

**The Vice-President and Minister for Finance (Mr. Kibaki):** On a point of order, Mr. Deputy Speaker. I have been in this House since 1963. Is it anywhere in our Standing Orders that an hon. Member can demand to be listened to regardless of whether he is speaking something worth listening to? Can you guide us, Mr. Deputy Speaker, Sir? I am asking for guidance because I have never heard of what the hon. Member is saying.

**Mr. Deputy Speaker:** Unfortunately, he must have forgotten our Standing Orders.

**Mr. Munyasia:** Bw. Naibu Spika, ingawa ninatoka heshima kubwa kwa Makamu-Rais na Waziri wa Fedha, ninajua kuna Kanuni nyingine za Bunge zinazosema kwamba, "When a Member is speaking, the rest of the hon. Members must hear him in silence".

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** On a point of order, Mr. Deputy Speaker. Could the hon. Member tell us which Standing Order says that, "When a Member is speaking, he must be listened to in silence?" That one is only provided under Standing Order No. 68 when a Member stands on a point of order but not when he is speaking.

**Mr. Munyasia:** Bw. Naibu Spika, sijui ni kwa nini Mhe. Mbunge wa Butere hakunisikiliza vizuri. Kuna Kanuni ya Bunge inayosema kwamba wakati Mhe. Mbunge anapongea, pasiweko na makelele mengi bali asikizwe kwa utulivu. Kwa hivyo, ningetaka kuendelea kutoa hotuba yangu.

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** On a point of order, Mr. Deputy Speaker. Could the hon. Member tell us which Standing Order is this? We would like to learn too, Mr. Deputy Speaker. All I know is that when it comes to a point of order, under Standing Order No. 68, is when an hon. Member should be heard in silence. It is not mentioned anywhere in our Standing Orders that when a Member is speaking, he must be heard in silence. If there is too much noise, a point of order may be raised by another Member drawing the attention of Mr. Speaker that there is too much noise, but there is no Standing Order, as he is stating. If there is one, let him tell us.

**The Assistant Minister for Health (Dr. Wameyo):** Quote it or withdraw the remark.

**Mr. Deputy Speaker:** Well, it does appear that it is not mentioned anywhere here, neither is it mentioned that if a Member is on a point of order, he has to be listened to in silence. Maybe that one has got to be included but as of now, it is not included here.

**Mr. Munyasia:** Bw. Naibu Spika, ningetaka kuendelea na mambo niliyokuwa nikizungumza. Haja yangu ilikuwa ni kuomba msaada kwa Kiti kinilinde kutokana na makelele yanayoendelezwa ili Makamu-Rais na Waziri wa Fedha aweze kusikia yale mambo ninayoongea juu ya fedha.

Nilikuwa nikisema kwamba Serikali yetu inafanya kazi nzuri kwa kutafuta pesa katika nchi za nje ili tuendeleze mipango ya maendeleo, kama mipango ya maji. Nilikuwa nikisema kwamba ikiwa ni mkopo wa kuendeleza mpango wa maji, wale wanaotupatia msaada huo wasifuatilie pesa hizo wakitaka kujua tutazifanyia kazi namna gani, Ni heri watuachilie mbali ili sisi wenyewe tutayarishie mipango yetu bila kuingiliwa. Hatungetaka wazifuatilie pesa hizo na kuzitumia.

Bw. Naibu Spika, ingefaa tuwe tukitayarisha mipango kikamilifu. Kwa mfano, kama ni Mto Athi ambao tungependa tutumie maji yake katika mwaka wa 1982 kwa mpango fulani, ni lazima tuangalie na kuona kwamba tutatumia pesa na kuendeleza mpango huo kikamilifu. Hakuna haja kumaliza wakati kwa mambo ya uchoraji tukitaka kujua maji yatakawenda namna gani. Huku ni kuharibu wakati.

**The Assistant Minister for Health (Dr. Wameyo):** Hapana!

**Mr. Munyasia:** It is true. Kuna Mhe. Mbunge mwingine anayesema "Hapana!" Sijui ni kwa nini Mhe. daktari anasema hivyo. Kwa mfano, Mtukufu Rais mwenyewe alikuja kwangu, Kyaani Matinyani, na akaendeleza uzuiaji wa mmomonyoko wa udongo bila kuwako na mpango wowote. Hapakuwako na mpango ulioonyesha ni lazima gully, au mfereji urekebishwe kufuatana na mchoro fulani. Mifereji ilikuwa ikitengezwa na sasa ukienda huko, utakuta kwamba maji yanazuiliwa. Lakini kama tungewapatia watu kazi hiyo, ingechukua miaka mitatu kutayarisha michoro jambo ambalo lingechukua pesa za bure. Kwa hivyo, mambo mengine ni ya upuzi.

**The Minister for Livestock Development (Dr. Mango):** On a point of order, Mr. Deputy Speaker. Is it in order for the hon. Member to suggest that we go back to the stone age whereby we should do things without plans at all?

**Mr. Munyasia:** Bw. Naibu Spika, sijui ni kwa nini Bw. Waziri huyu haelewi vile ninavyosema. Ninasema kwamba—ningetaka anisikilize kwa makini—pesa tunazokopa zisifuatiliwe na wale watu wanaotukopesha kwa kusema, "Ni lazima tutayarishie michoro, au feasibility studies". Ikiwa tumekopa pesa za kuendeleza mpango fulani, wale watu wanaotukopesha wasifuatilie wakitaka tufuate mpango wa michoro yao.

**The Minister for Urban Development and Housing (Mr. Rubia):** We do not follow you!

**Mr. Munyasia:** Well, thank you "Mr. Charles".

Bw. Naibu Spika, nilikuwa nikisema kwamba huko ni kuharibu wakati.

**Mr. Kitele:** On a point of order, Mr. Deputy Speaker, is it in order for hon. Munyasia to say "Thank you, Mr. Charles" instead of saying, "Thank you hon. Charles"?

**Mr. Munyasia:** Ni kweli, ningesema Mhe. Charles. Anyway, he is my friend. Kwa vile hajalalamika, sijui jambo hili linamhusu Mhe. Mbunge wa Iveti North kwa njia gani. Pilipili usioila yakuwashia nini?

**Mr. Deputy Speaker:** Order! Mhe. Kitele ana haki kuona kwamba tunafuata Kanuni za Bunge hili. Hiyo ndiyo sababu alisimama kwa jambo la nidhamu.

**Mr. Munyasia:** Mhe. Charles Rubia, ahsante sana kwa kuniongoza kidogo.

Bw. Naibu Spika, nilikuwa nikisema kwamba—Waziri wa Ustawi wa Mifugo hakunieleza—tunapokopa pesa kutoka nchi za ng'ambo, watu wengine wanaotukopesha pesa hizo hutaka kuzifuatilia wakitaka wafanye uchunguzi kwa kutayarisha michoro, jambo ambalo huwa-wezeshia wamalize pesa zote kwa mipango ya michoro. Nilitoa mfano wa "Sh. 200" zilizotolewa kwa mipango ya maji huko Machakos, lakini ukienda huko, huwezi kujua pesa hizo zilifanya kazi gani.

**An hon. Member:** Sh. 200!

**Mr. Munyasia:** No, Sh. 200 million. Ukienda huko Machakos, Bw. Naibu Spika, huwezi kuona kitu chochote kinachonyesha kuwa pesa hizo zimetumika. Hii ndiyo sababu nilisema kwamba wakati mwingine tunaharibu wakati kwa mipango ya uchoraji tunapowaleta hapa nchini wataalamu watuambie ni vipi tunaweza kutumia maji ya mto fulani. Sisi wenyewe tunaweza kujifanyia kazi ya uchoraji na kuhifadhi maji ya mito fulani. Hapo ndipo nilipotoa mfano wa Mtukufu Rais alipoitembelea sehemu yangu. Alituingoza kwa kufunga gullies zote na sasa ukienda huko, utakuta kwamba kuna maji na mimea inakua vizuri. Hapakuwako na kazi ya uchoraji wakati tulipokuwa tukizuia mmomonyoko wa udongo. Kama watu wengine wangeambiwa waende kuchunguza vile zile gullies zingerekebishwa, wangeanza kutayarisha michoro yao na kumaliza wakati na pesa. Kwa hivyo, ni lazima kuweko na mpango kamili wa kuona kwamba maji ya mito yanahifadhiwa, miti ipandwe kando kando ya mito ili maji yasipotee bure. Tukifanya hivyo, tutaona kwamba hakutakuwako na upungufu wa chakula nchini.

Bw. Naibu Spika, nchi ya Kenya ni ya kilimo na imefanikiwa kwa mambo mengi. Kwetu Ukambani ardhi yenyewe—

**The Assistant Minister for Health (Dr. Wameyo):** Hakuna mvua.

**Mr. Munyasia:** Mhe. daktari anasema kwamba hakuna mvua. Hayo ni majaliwa ya Mungu. Today it is me, tomorrow it is you. Kuna mvua Ukambani na ningetaka Mhe. daktari ajue hivyo. Vile ninavyosema ni kwamba ni lazima kuweko na mpango wa kuona kwamba maji yote yanayotoka mbinguni yanazuliwa yasiitiririke katika bahari ya Hindi. Hivi majuzi tulipozitembelea nchi za Philippines na Thailand tuliona kwamba maji yamejaa katika nchi hizo na mpunga

unakuzwa kwa wingi. Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika, ningetaka kukuhakikishia kwamba maji ya mito yote ya Ukambani yakihifadhiwa, Ukambani inaweza kuilisha Kenya nzima kwa chakula. Hakuna mtu yeyote anayeweza kuniambia Ukambani haiwezi kufanya hivyo kwa sababu ardhi ni nzuri na ni utaalumu tu ambao umekosekana.

Bw. Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, ningetaka Waheshimiwa Wabunge watakapata nafasi kesho, waende Ukambani kujionea vile Masinga Dam ilivyojengwa. Kesho Mhe. Biwott atamkaribisha Mtukufu Rais huko Masinga Dam na ingekuwa bora kama Waheshimiwa Wabunge wangeenda huko kujionea vile mambo yalivyo. Wakienda huko, wataona kwamba bwawa hilo lilijengwa katika sehemu kavu, lakini sasa mahali hapo panaonekana kama ni bahari. Hili ni bwawa la pekee katika Africa Mashariki kwani lina umbali wa kilomita 52. Ni kwa nini mipango isitayari-shwe ya namna hii nchini kote ambako kuna mito ili kuhifadhi maji yanayoweza kutumiwa kwa mipango ya kunyunyizia mashamba maji? Nchi hii itajipatia chakula kingi ikiwa tutatumia mpango wa kunyunyizia mashamba maji. Maji ya mito yakihifadhiwa, tutapata nafasi ya kupanda mimea mbali mbali kwa wingi—yaani, cash crops kama maembe, michungwa, mapapai, cashewnuts, pilipili, na kadhalika—na kujipatia pesa za kigeni baada ya kuuza bidhaa hizo katika nchi za ng'ambo. Lakini kama hatuna mpango kamili, kila wakati kutakuwako na njaa.

Bw. Naibu Spika, singetaka kuendelea sana kuzungumzia jambo hili. Kitu ambacho nilitarajia kusisitiza katika Hoja hii ni kwamba ni lazima mambo yapingwe kwa njia kamilifu kwa kuona kuwa maji ya mito yote yamehifadhiwa.

*(Several hon. Members rushed into the Chamber)*

**The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku):** On a point of order. What is happening, Mr. Deputy Speaker? Is the House burning?

*(His Excellency the President entered into the Chamber and took his seat as the Member for Baringo Central)*  
*(Applause)*

**Mr. Munyasia:** Bw. Naibu Spika, ningetaka kuchukua nafasi hii kutoa shukrani kwa Mtukufu Rais kwa kuingia Bungeni na kushirikiana nasi katika majadiliano. Mtukufu Rais amekuja hapa kutusikiliza, kama watoto wake, tukiongea juu ya matatizo yanayotandaa kuhusu upungufu wa chakula. Kwa hivyo, ninasema ahsante sana kwa Mtukufu Rais. Ninawomba Mungu ampatie maisha marefu ili aendelee kuwatembelea watoto wake.

*(Applause)*

Nafikiri kwamba Mtukufu Rais atanisamehe, nikipitia kwa Kiti, ili nipate kuendelea na yale mambo nilikuwa nikisema.

Bw. Naibu Spika, nilikuwa nikisema kwamba mpango mzuri ni lazima ufanywe kama vile Serikali ilivyo-fanya hapo mbeleni na kama inavyoendelea kufanya, wa kujenga mabwawa ya maji. Nilianza kule Kamburu, Gitaru na sasa tuko na Masinga Dam ambapo nasikia kwamba Mtukufu Rais atakwenda kesho kufungua rasmi mpango huu wa maji. Nilisema kwamba

[Mr. Munyasia]

mahali pale palikuwa pakavu sana na ule mto ulikuwa bila maji na palikuwa mawe tupu na pale palikuwa sehemu ambapo binadamu hawezi kuishi, lakini ukifika kule sasa, mambo yamebadilika. Hii ndiyo sababu nilitoa mwito kwa Waheshimiwa Wabunge ambao watapata nafasi kesho, waende wakajionee wao wanyewe kwamba nchi ikitengenezwa jinsi hii inaweza kuwa pahali pazuri pa kuishi. Ie dam inatumiwa kupeleka maji umbali wa kilomita karibu 52 katika upande wa Embu. Hii ndio sababu nilisema kwamba ni lazima mpango kamili ufanywe ili mito mingine ambayo inaweza kuzuliwa, iweze kutumiwa, ili maji hayo yatumiwe katika mipango ya kunyunyizia mashamba maji. Hii ndiyo njia ya pekee ambayo inaweza kutumiwa ili nchi hii yetu iweze kujitegemea kwa chakula na kuhakikisha kwamba hatukimbii katika nchi za ng'ambo kutafuta msaada wa chakula.

Pia, Bw. Naibu Spika, ningetaka kutoa shukrani kubwa kwa Mtukufu Rais kwa vile wakati tulipokuwa na njaa alikimbia katika nchi za mbali ili kwenda kutuletea chakula. Hiyo ni heshima kubwa sana kwake na hii ndiyo sababu nasisitiza kwamba hatutaki kuona Mtukufu Rais wetu, kwa ajili ya unyonge wetu, na kwa kutofikiria kufanya mipango yetu, aende tena kule kutafuta chakula, hali Mungu ametupatia mvua ya kutosha, na maji yanakwenda katika Bahari ya Hindi. Ni lazima tuyazuie haya maji na kuyatumia katika mipango ya kunyunyizia mashamba yetu maji ili nchi yetu iweze kujitegemea kwa chakula.

Bw. Naibu Spika, kwa haya machache, naunga Hoja hii mkono.

Mr. Boy: Ahsante sana, Bw. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili nami pia niseme machache juu ya Hoja hii ya chakula. Kabla ya kusema chochote, ningetaka kuchukua nafasi hii pia kumshukuru Mtukufu Rais kwa kuwa nasi katika Bunge hili tukufu leo, ili asikilize wakati watoto wake wanapojadiliana mambo yanayohusu chakula nchini Kenya. Sisi tunamwomba Mtukufu Rais maisha mema na tunatumaini kwamba mara kwa mara ataweza kututembelea hapa ili aweza kutusikia kwa kinaganaga tunapozungumza juu ya mambo ya nchi nzima kwa jumla. Bw. Naibu Spika, unaweza kunilinda kutoka kwa Mhe. ole Oloitipitip.

Mimi ningetaka kusema maneno machache tu juu ya Hoja hii. Kwanza, ningetaka kumshukuru Mtukufu Rais kwa juhudi kubwa aliyofanya, na pia kwa hatua kubwa aliyochukua ya kuzuia magendo nchini Kenya. Nasema hivyo kwa sababu kuna chakula kingi ambacho kinakuzwa na watu wa Kenya. Inajulikana dhahiri kabisa kwamba watu wa Kenya ni watu wanaofanya kazi kwa nguvu zaidi na wanapenda kulima sana lakini jirani wetu ambao wanaona taabu wanapolima kwa sababu wana uvivu na siasa nyingi, wanafanya kazi kidogo sana. Kwa hivyo, vyakula kutoka nchini Kenya vinachukuliwa na watu wengine wanaotaka utajiri wa haraka. Kwa hivyo, wanakwenda kuuza chakula katika nchi jirani na jambo hili ndilo limetufanya sisi katika nchi hii kukumbwa na njaa kubwa mwaka uliopita. Mtukufu Rais alikuchua hatua ya kuona kwamba mtu

yeyote atakayepatikana akifanya magendo, atachukuliwa hatua, na kwa kusema kweli jambo hili limeangaliwa sana katika Kenya na sasa hakuna magendo. Wale waliokuwa wakifikiria kwamba hayo yalikuwa maneno tu ya mdomo, walijaribu na wakaona cha mtema kuni. Sasa nchi iko katika hali njema zaidi kwa sababu Mungu ametuletea baraka ya mvua na watu wa Kenya wanalima sana chakula katika nchi hii. Kwa vile Mtukufu Rais yuko hapa, tungetaka kusema kwamba ule mkazo wa wale watu wanaotaka kutajirika kwa haraka sana, unafaa kushikiliwa hivyo hivyo. Tungetaka Mtukufu Rais aushikilie mkazo huu hivyo hivyo, ili hatua kali ichukuliwe kwa mtu yeyote ambaye anataka kupeleka chakula katika nchi nyingine ili awe tajiri haraka. Tungetaka hatua kali ichukuliwe ili chakula kibakie hapa kwetu Kenya.

Pia, ni lazima mipango kamilifu ya kunyunyizia mashamba maji ifanywe na vile vile mipango yote ya kilimo, ni lazima itiliwe nguvu ili kuweza kuwasaidia watu ambao wana taabu juu ya kilimo. Kuna nchi nyingine ambapo watu hawawezi kunyunyizia mashamba maji kwa sababu maumbile yake yana milima, mito na hali ya hewa ni nzuri na watu hulima sana. Lakini kuna sehemu nyingine ambazo ni kavu sana ingawa watu wengi wanalima kwa bidii sana, lakini kwa sababu ya hali ya hewa vyakula havikui vizuri.

Ni lazima Wizara ya Kilimo ihakikishe kwamba zile sehemu kavu ambapo watu wanataka msaada, zinasaidiwa ili watu waweze kusaidiwa katika mambo ya chakula. Pia, ni lazima Wizara hii ihakikishe kwamba watu wanalima kwa wingi sana kama inavyofanya katika mahali pengine. Vile vile, tungetaka mipango ya kunyunyizia mashamba maji ianzishwe katika sehemu nyingine, kwa mfano, kule pwani. Kuna watu wengine kule ambao wanakuza mpunga kwa kuyatumia maji yanayotiririka kutoka sehemu ya Tanzania na ingekuwa jambo la busara kama maji haya yangetumiwa katika mipango ya kunyunyizia ili tuweze kupanda vyakula vingi sana katika mashamba yetu. Nasema hivyo kwa sababu mpunga umekuwa taabu sana kupatikana katika sehemu ya Kwale na Vanga. Mpunga ukikuzwa, unapatikana kwa wingi na hata Waziri wa Kilimo anaelewa hivyo sana, lakini kwa sababu ya kukosa mipango ya kunyunyizia mashamba maji, imekuwa ni taabu sana kukuza mpunga. Sasa mtu akipanda mpunga, anapata tu kama gunia 30, 50 au 60 na hii ni kosa kulingana na ukulima wa kule kwetu. Lakini kama mpunga unakuzwa kwa njia nzuri, chini ya mpango wa kunyunyizia mashamba maji, unaweza kupatikana kwa wingi sana katika sehemu hii ya pwani. Mimi najua kwamba Waziri anaelewa hivyo kwa sababu amezitembelea sehemu hizi na tunamshukuru sana kwa jambo hili. Tumeona juhudi ambazo amefanya za kurwasaidia watu katika sehemu hizi na tunaishukuru sana Serikali kwa bidii hii, lakini kwa sababu ya ukame ambao sasa imekuja, tungetaka juhudi hizo ziongezwe zaidi ili watu waweze kulima vizuri.

Pia, Bw. Naibu Spika, wakati mwingine tunafikiria kwamba mahindi ndio chakula cha pekee cha nchi hii. Hata mihogo ni vyakula vya watu na ni lazima ukuzaji wa mihogo utiliwe nguvu. Watu wengine wanasema,

[Mr. Boyl]

"Sipendi mihogo, hafadhali mahindi au ngano au njugu", lakini mihogo ni chakula kizuri na kwa hivyo, ni lazima ukuzaji wa mihogo utiwe nguvu ili watu waikuze na kupata chakula. Kwa hivyo, ni lazima chakula hiki kitilwe nguvu, na sio kwa kusema ati mihogo inaweza kutengeneza biskuti au itapelekwa Ujerumani au Uchina hapana, lakini inaweza kutusaidia katika mambo ya chakula chetu hapa nchini. Pia, nafikiri kwamba Wizara inayohusika na mambo ya ardhi haifanyi kazi vizuri na mambo yake yanazoroteka sana kwa sababu wakati mwingine ardhi inapimwa lakini cheti cha kumiliki ardhi hiyo kinacheleweshwa sana. Mkulima mwenye ardhi ile akiomba mkopo ili aweza kununua vifaa vya kisasa au ili aweze kununua mbolea au vitu vingine, anaona taabu kupata mkopo kwa sababu anautilizwa, "leta title-deed yako", lakini yeye hana title-deed. Utaona kwamba mashamba yalipimwa miaka mingi iliyopita, lakini watu hawawezi kupata title-deed. Unapokwenda kule ofisini, unaambiwa, "fulani amekwenda livu". Mimi naunga mkono matamshi ya Mtukufu Rais ya hivi juzi alipotoka safarini kwamba mfanyakazi yeyote wa Serikali atakayezorotesha mambo, atamfuta kazi. Mimi namuunga mkono Mtukufu Rais kabisa. Futa yeye ikiwa hataki kufanya kazi. Nasema hivyo kwa sababu kuna watu wengi wanaoketi katika district development committees, lakini pesa zinrudishwa Treasury bila kufanya kazi. Watu wanaotaka title-deeds, hawapati title-deeds na ukiuliza ni kitu gani kinachoendelea, unaambiwa, "fulani hayuko", au "fulani amekwenda huko au kule". Ukifika kule utaona mambo ya ajabu sana ma watu hawapati title-deeds zao. Kwa hivyo, ni taabu kwa mkulima kutoka pwani kupata mkopo kwa sababu anaambiwa atoe title-deed yake, na yeye hana title-deed. Ili kilimo kipatikane kwa haraka sana na ili kila mkulima ajitegemee mwenyewe, juu ya mambo ya pesa na kadhalika, tunataka land adjudication iharakishwe ili mambo ya vyeti vya kumiliki ardhi yakamilishwe ili watu waweze kupata msaada wa mkopo, kwa sababu watu wa pwani kwa jumla hawana pesa. Kwa hivyo, tungetaka kuona Wizara inayohusiana na mambo ya ardhi ikihakikisha kwamba vifaa kama hivyo vinapatikana kwa sababu watu wa Kenya wanafaa kusifiwa sana kwa sababu wao ni wakulima sana, na kwa sababu kuna mvua kidogo wanafanya kazi kwa bidii sana.

Kwa hivyo, mimi sina mengi ya kusema zaidi kwa sababu mimi naona kwamba Hoja hii ni straightforward. Lakini tungetaka kuisitiza kwamba Serikali ijaribu kuzisaidia zile sehemu kavu kwa msaada wa Serikali ili wananchi katika sehemu hizo waweze kupata mavuno mema.

Kwa hayo machache, naunga mkono.

**The Minister for Local Government** (Mr. ole Oloitipiti): Ahsante sana, Bw. Naibu Spika kwa kuni-patia nafasi hii. Mimi niko na furaha kubwa sana kwa kupata nafasi hii ili kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamepata nafasi ya kuzungumza juu ya Hoja hii. Sisi Wabunge wote tunasema kwa nguvu na kwa moyo yetu yote kwamba tuna furaha kubwa sana kwa Mtukufu Rais wetu kuingia hapa Bungeni kwa ghafula; katika Bunge hili Tukufu

la Taifa tukizungumza mambo ya nchi hii. Tunarudisha shukrani nyingi sana kwa Rais wetu kwa kuweza kutufikia leo. Jambo la pili ni kwamba kwa niaba ya Wabunge wote, na ninavyosema hivyo najua ni kweli, sisi sote tunamwambia Rais wetu kwamba tuna imani na yeye. Na imani yetu kutoka kwa sisi Wabunge inamwelekea yeye, President Moi, directly. Nimesema hapo mbeleni kwamba loyalty yetu haigawanywi na inatoka kwetu na kumwelekea directly na sasa iliyobaki ni Wabunge kutia sahihi na kusema halleluyah. Tumekwishasoma historia, na pia tumekwishana Marais wengi ambao wamechaguliwa katika nchi za Bara la Afrika ambazo zimepata Uhuru, lakini hatujapata kusikia Rais ambaye anakwenda katika Bunge kama huyu Rais wetu. Jambo hili linaonyesha kwamba Rais wetu ana imani na Wabunge wake na pia ana imani na nchi yake ambayo anaiongoza. Anataka kuja hapa Bunge kusikia mwenyewe vile tunavyosema hata kama akikaa kule State House, ana chombo cha kusikiliza na kujua ni kitu gani tunachosema, lakini yeye alikuwa anataka kuja hapa kujionea yeye mwenyewe na kujua ni mambo gani tunayosema hapa Bungeni. Lakini alitaka tu kuja hapa kufanya a physical check ili aweze kuona vile nyuso zetu zilivyo hapa Bungeni. Kwa hivyo, hata mimi mwenyewe nashukuru kwa sababu ametukuta sisi sote tukiwa hapa Bungeni.

(Applause)

Kwa hivyo, kwa kuwa Rais wetu ni mtu anayemcha Mungu, na kwa vile sisi watu wa Kenya pia ni watu wanaomheshimu Mungu, ningependa kusema kwamba sisi tunamheshimu Rais wetu na taifa letu la Kenya. Kwa hivyo, Mtukufu Rais tunasema ahsante sana kwako kwa kuja katika Bunge siku ya leo.

Jambo la pili ambalo ningependa kutaja, Mtukufu Rais, ni kwamba dakika chache zilizopita Wabunge wako wamewaokoa wananchi kutoka kwa minyororo ile ya kunyanyaswa ambayo wewe mwenyewe umekuwa ukihusika sana nayo. Tumeupitisha Mswada unao-husika na mambo ya ardhi ili kesi zinazohusika na mambo ya ardhi zisiende tena kwa mawakili na kuwafanya wananchi wa Kenya kulipa pesa ambazo hazina maana kwa mtu ambaye hajui matatizo ambayo wananchi walio nayo juu ya ardhi. Kwa hivyo, leo tume-yarudisha mamlaka hayo kwa wananchi wenyewe.

**An hon. Member:** Kwa wazee.

**The Minister for Local Government** (Mr. ole Oloitipiti): Ndiyo, kwa wazee wale wa vijiji ambao wanaweza kuziamua kesi kwa njia ya haki kwa sababu wanajua ukoo na milango ya watu. Wazee kama hao ndio wanaojua ni nani aliyekuwa baba ya mtu fulani, au ukoo ambako mama yake alitoka, na heshima gani, ama urithi gani waliokuwa nao. Mtukufu Rais, tume-uitikia ule mwito wako kwamba ni heri jambo hili litoke mikononi mwa mawakili.

Kwa hivyo, ningependa kukuambia, Mtukufu Rais, kwamba tumeupitisha Mswada huo sasa hivi. Kitu ambacho tunakuomba ufanye, Mtukufu Rais, ni kwamba Mswada huu ukifika kwako, ni heri utoe kibali-chakor juu yake kwa kuweleka sahihi kwa sababu it is your own baby ili uwe mwisho wa barabara kwa wale mawakili ambao wamekuwa wakiwanyanasa

[The Minister for Local Government]

wananchi. Kwa hivyo, Mtukufu Rais, namuomba Mungu akupatie maisha marefu na uongozi mwema kama kawaida.

Nikiendelea, ningependa kusema machache juu ya chakula. Ni lazima tuzungumze tena juu ya jambo hili kwa sababu hukuwa hapa, Mtukufu Rais. Tumekuwa tukizungumza juu ya jambo hili kila mahali, na ume-kuwa ukiyasikia yale ambayo tumekuwa tukizungumzia, kwa kusema kuwa nchi hii ya Kenya na Wabunge wako wana shukrani tele kwako kwa kazi ambayo ulifanya ili kutuokoa kutokana na njaa tuliyoukuwa nayo wakati uliopita. Tunakushukuru sana kwa kazi hiyo, Mtukufu Rais. Wakati tulipokuwa na njaa, hukulala; ulikuwa ukienda Marekani, Ufaransa na mahali pengine kwa sababu ya sisi sote. Pia, kutokana na juhudi zako, na baraka za Mwenyezi Mungu, tumewahi kupata mvua na sasa tuna chakula cha kutosha katika Kenya. Kwa hivyo, tungependa kusema ahsante sana kwako.

Nikiendelea, ningependa kusema machache juu ya Hoja hii, ningemuomba Waziri anayehusika ayasikie yale nitakayosema. Kwa kuwa sehemu ninakotoka ni kavu kidogo, tunataka kutia maanani hasa katika zile sehemu za Kenya ambazo ni kavu. Katika sehemu ya Kajiado tunakotoka, tuna mito mingi kama Anoldures, Akimana, Asinet na Mburong ambayo maji yao yanatiririka bure na hali maji kama hayo yanaweza kutumiwa kwa mpango kama ule wa Tana River Development Authority. Kwa hivyo, ningemuomba Waziri anayehusika na mambo haya awe na mpango kama huo katika sehemu ya Kajiado.

Bw. Naitu Spika, Waisraeli wamekwishaitembelea sehemu hiyo na wakasema kuwa watatupatia \$300,000 ambazo zinaweza kutumiwa katika mpango wa kunyunyizia mashamba maji, na kwa hivyo, kitu ambacho wanataka tufanye ni kuwa na feasibility study ili tukishafanya hivyo waweze kuanzisha mpango huo wa kunyunyizia mashamba maji. Tumekwishapiga ripoti zetu kwa Waziri anayehusika na mambo haya na kilichobaki ni kukuomba, Mtukufu Rais, kama tuna-weza kupata njia yoyote ya kupata Sh. 4,000,000 ili kazi hiyo ianze halafu wananchi wapate nafasi ya kunyunyizia mashamba yao maji na kukuza vyakula kwa wingi. Tunataka mpango huo uwe wa kudumu. Kwa kuwa vitunguu na vitu vingine hukuzwa kwa wingi katika sehemu yetu, tungependa kukuomba uliangalie jambo kama hilo.

Nikizungumza juu ya kunyunyizia mashamba maji, sizungumzi juu ya sehemu ya Masai peke yake, nazungumza juu ya sehemu kama ya Yatta anakotoka Mhe. Munyasia na sehemu nyingine ambazo zimechukuliwa chini ya Tana River Development Authority. Pia, ningemuomba Waziri aone kwamba kila wilaya, au kila sehemu, iliyoko kavu na ambayo iko chini ya Tana River Development Authority ina wawakilishi wake katika bodi hiyo ili wawakilishi hao waweze kusema ni pahali gani panapofaa kuanzishwa kwa mpango wa kunyunyizia mashamba maji. Nasema hivyo kwa sababu si jambo zuri kwetu kuendelea kuomba Rais wetu kwenda kuomba chakula kutoka

katika nchi nyingine na hali tuna ardhi; ni lazima sisi wenyewe tufanye kazi katika ardhi hii ili tuweze kupata chakula cha kutosha. Ikiwa tuna nchi ya Kenya katika roho zetu, ningependa kusema kuwa wakati umefika ambapo ni lazima tuone kwamba tunafanya kazi katika Serikali hii ya Nyayo ambayo tunajivunia kwamba tuko ndani yake kabisa kabisa. Kwa hivyo, kunyunyizia mashamba maji katika sehemu kavu ni kitu kikubwa sana ambacho kikifanywa, nina hakika kwamba wananchi wanaweza kufurahishwa nacho.

Nikiendelea, siwezi kusahau kusema kwamba ni lazima mipango ya kunyunyizia mashamba maji iendeshe pamoja na upandaji wa miti katika nchi yetu tukufu. Ikiwa kuna mpango wa kunyunyizia mashamba maji mahali pengine, ni lazima mpango huo uendeshe pamoja na upandaji wa miti ili tuweze kuzuia kuenezwa kwa jangwa katika nchi yetu tukufu.

Jambo langu la nne ni juu ya ng'ombe. Nafurahi sana kwa sababu Waziri wa ng'ombe, au Waziri wa mifugo yuko hapa.

An hon. Member: Hatuna Waziri wa ng'ombe.

The Minister for Local Government (Mr. ole Oloitipitip): Yeye ni Waziri wa ng'ombe, au Waziri wa mifugo.

The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku): Jambo la nidhamu. Je, ni haki kwa Mhe. Waziri kulipotisha Bunge hili kwa kutubandika jina "Waziri wa ng'ombe" ambalo haliko? Wizara yetu ni Wizara ya Ustawi wa Mifugo wala sio Wizara ya ng'ombe.

## COMMUNICATION FROM THE CHAIR

### WELCOME TO HIS EXCELLENCY THE PRESIDENT

Mr. Deputy Speaker: Order, order. Hon. Members, before I reply to the point of order which has been raised by the hon. Assistant Minister, it is my great pleasure, on your behalf, and on my own behalf, to warmly welcome the presence of His Excellency the President and Commander-in-Chief of our Armed Forces, Mhe. Daniel arap Moi, and I would like to assure him of our total loyalty, commitment and dedication to follow diligently his Nyayo philosophy which we believe and uphold as a sure way to develop this nation to greater prosperity.

(Applause)

May I also, on your behalf, wish His Excellency the President a very happy Christmas and a prosperous New Year.

(Applause)

The Assistant Minister for Livestock Development (Mr. Shikuku): Jambo la nidhamu, Bw. Naitu Spika. Nilisimama kwa jambo la nidhamu kuuliza kama ni haki kwa Waziri kutuita, au kusema kuwa Wizara yetu ni Wizara ya ng'ombe. Je, ni haki kwake kuita Wizara yetu Wizara ya ng'ombe na hali Wizara yetu inajulikana kama Wizara ya Ustawi wa Mifugo? Wizara yetu inajulikana kama Wizara ya Ustawi wa Mifugo wala sio Wizara ya ng'ombe, kwa sababu tunawangalia hata punda.

(Laughter)

**The Minister for Local Government** (Mr. ole Oloitipitip): Bw. Naibu Spika, ikiwa hiyo imemuumiza rafiki yangu, ningependa kumwambia kwamba hiyo haikuwa nia yangu. Lakini livestock development maana yake ni ustawi wa mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na hata kuku. Lakini ningependa kukuomba unisamehe juu ya jambo hilo kwa sababu mimi kama Mmasai nafikiria ng'ombe peke yake.

*(Laughter)*

Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika, nilikuwa nikisema kwamba wananchi kwa jumla wamefanya bidii kujijengea vidimbwi vya kuwaogeshea ng'ombe.

Lakini tumepata fununu kwamba Wizara hiyo itafanya jambo fulani kuwaasaidia ng'ombe. Kama itafanya, ninafikiri wakati umefika kwao sasa kutujengea dips. Hata kama tutalipia madawa au kufanya mambo mengine kwa njia nyingine si vibaya. Lakini tunataka kote katika Jamhuri ya Kenya kuliko na ng'ombe watu wapate vidimbwi vya kuwaogeshea ng'ombe.

Si pahali pa kuogeshea ng'ombe peke yake kwa sababu tungetaka pia tujenge na Serikali yetu tukufu kliniki ambako mwananchi anaweza kwenda kwa urahisi kununua madawa hayo. Hii ni kwa sababu nikitoka mfano katika Kajiado District, ukuta kutoka Oloitokitok ni maili 181 mpaka Kajiado. Madawa yako Oloitokitok na Kajiado peke yake. You imagine, mtu kusafiri katikati hapo maili 80 kwenda kutafuta madawa. Hiyo ni gharama kubwa.

Kama ni close administration ambayo tunataka ni lazima sisi tuone kwamba jinsi binadamu anavyotaka kliniki nao ng'ombe wetu wanataka kuwa na kliniki ambako tutakuwa tukinunua madawa hayo. Pia tungetaka upatiwe wale madaktari ambao ukiwaita usiku wanaweza kujua ng'ombe huyo ana ugonjwa gani. Hii ni kwa sababu ni vigumu sana kwa mtu wa kawaida kujua ng'ombe huyo ana anthrax, Foot-and-Mouth disease, Rinderpest, au East Coast fever.

**An hon. Member:** Pleural-pneumonia.

**The Minister for Local Government** (Mr. ole Oloitipitip): Na Pleural-pneumonia. Hiyo ni shida. Atakayejua hivyo, ni mtaalamu. Kwa hivyo, ninasema kwamba ikiwa tunajenga dispensari za binadamu na binadamu anaishi kwa kuwa na chakula, hao ng'ombe pia wanahitaji kliniki. Kwa hivyo, tungetaka Waziri afanye kazi kuanzia juu mpaka chini ili aweze kuona kwamba kila kitu kinafanyika.

Pia kuhusu yale madawa tunayotia katika dips zetu tabu ya wananchi leo ni kwamba hatuna wale dip-attendants ambao wanajua kazi hiyo. Unaweza kuweka mtu kama dip-attendant, lakini hajui ni siku ngapi darwa fulani italkaa kabla ya kupelekwa katika Kabete Laboratories ambako tuna pahali pa kipekee pa kupima madawa hayo katika Kenya. Hata ikiwa ni kutoka Kitui, ni lazima madawa yaletwe hapa Nairobi. Tungetaka hizi laboratories pia ziwe karibu katika kila wilaya ambako kazi hiyo itafanyika.

Jambo la mwisho ni kuuliza wakati ambapo tuna ukame kama huu pahali ambako hatuna maziwa sasa tusaidiwe na magari ambayo yanasafinisha maziwa kwa sababu sehemu hizo zimekuwa kavu. Tungetaka maziwa

ya Kenya Co-operative Creameries yaende Masaini, Samburu, Kitui na Meru. Labda watu wa Meru wana barabara na pengine wao ni sawasawa. Lakini tungetaka kumuuliza Mhe. Shikuku ambayo ni Waziri Msa-idizi mwenye nguvu ahakikishe kwamba yale maziwa ambayo tunanunua hapa yapelekwe huko ili Wamasai na Wakamba wasikose maziwa kwa sababu sehemu zao zimekwishakauka. Tungetaka apeleke maziwa hayo huko na tutayanunua. Hatutaki kupewa maziwa bure; hakuna cha bure.

Jambo langu la mwisho ni juu ya district development committees. Tungetaka kusema kwamba kamati hizi zimebolewa na Serikali ili kuwasaidia wananchi. Lakini kwa kusema haki, wakati mwingine pesa zinairudi Hazina bila kutumiwa. Hii ni aibu. Kama Serikali yetu tukufu inatoa pesa kuwasaidia wananchi na projectis hazifuatwi, mimi ningetaka kuuliza Serikali na Waziri tuwe na inspector katika kila mkoa ambaye atakuwa akiangalia projects, A, B, C na D katika kila wilaya. Hii ni kwa sababu hata juu mimi nilihudhuria mkutano wa kamati ya maendeleo ya wilaya, na niliona kwamba mambo yamekwama mpaka nikapiga gari moto ili watu wainuke. Lakini ni siku ngapi mtu kama mimi au wewe atakwenda huko?

Kwa hivyo, tungetaka tuwe na mipango ya kuona kwamba pesa hizi za kamati za maendeleo za wilaya zikitolewa, zitumiwe kwa wananchi na tuwe na mtu wa kuangalia na kuona kwamba pesa hizo zimetumiwa kwa njia sawasawa sana.

Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono. Pia ninamshukuru Rais wetu na ninamwomba Mungu ambariki. Sisi sote tuko pamoja naye. Ahsante sana.

**His Excellency the President** (Mr. arap Moi): Mr. Deputy Speaker, Sir, my appearance in this House shows or indicates the importance I attach to the National Food Policy.

*(Applause)*

A nation which cannot feed itself, is not worth a salt. We take pride of ourselves if we can feed our people. A united country and united leaders can only succeed if they have that commitment. People who are on the job, whether Ministers, the President for that matter, or any other person without commitment, are not fit to be patriots.

*(Applause)*

Therefore, I support this Sessional Paper No. 4 of 1981 with some amendments which the Ministry is proposing to make. As you all know, my dear sisters and brothers, although I do not see sisters here today—

**Mrs. Onyango:** We are here.

*(Hon. Mrs. Gachukia and Mrs. Onyango stood up)*

*(Applause)*

**His Excellency the President** (Mr. arap Moi): My dear sisters and brothers, as you all know, we in this country, can succeed if our objective of improving the standard of life of our people can be fulfilled. I am happy with the way you are talking about things.

**[His Excellency the President]**

given that you have no ulterior motives. If your objective is that of making our common man improve his standard of living, then I entirely agree with you.

*(Applause)*

I have stated more than once that our youths must play a very important role in shaping the future and laying a firm foundation for our nation, so that the future can look bright. It is on this basis that we the older generation, should set a very good example to them. We should handle them humanly, and we should understand their feelings. If we do not understand their feelings, then we have not done our job.

*(Applause)*

We should not lament on their behaviours. I was impressed the other day when I met a club of youngsters in secondary schools who numbered 50,000 and who have come out to support the conservation of wildlife. This is an indication of what they want, but they want to be given a lead. The National Food Policy is governed by many factors such as productivity of the field officers; productivity of those in the officers; productivity of all officers in various departments working together for one common goal.

*(Applause)*

It should be understood that we have one Government, and that one Government has 25 Ministries. No one should say that "This is my Ministry" and run it as if he is a bull; not wanting other small bulls to come around!

*(Applause)*

We should combine our efforts, ideas and knowledge together, and that can form a solid foundation. No one person is a jack of all trades! I cannot pretend that I know everything. Each one of you can contribute immensely to the prosperity of this country if you try to do so. Each one of us ought to understand that we are on the run by virtue of the fact that we are producing children everyday, and those children number about 400,000 annually. That is our effort and that effort must be backed by enough food to feed them!

*(Applause)*

When I said that we must introduce primary school milk scheme, people were doubtful as to whether that would succeed. At the time we had about 200,000 litres of milk everyday. Now, we have 900,000 litres of milk; which is more than enough. So, my children are enjoying themselves and it is only fair if we can spend only K£10 million, my sisters and brothers, for feeding these children and they become healthy. Naturally, we will reduce the same amount of money by children not going to dispensaries and clinics to be cured of colds and so on.

*(Applause)*

These are the things people ought to know when producing these statistics. Therefore, as I said earlier on, the National Food Policy involves so many things. If we are to succeed in this scheme then we must make sure that the Ministries of Agriculture and Livestock

Development must help the smaller fellows who work around the country-side to meet the demands. They should be helped!

*(Applause)*

I have not yet seen what I indicated last time that I must see agricultural department people because if they have not been seen in any given area, then people will ask "Where are they?" But they do not want that because they do not want to be seen by people and, therefore, they do not want to be identified. They want to be out of the scene; receive their salaries at the end of the month and go back to their private businesses. Therefore, the output is nil!

*(Applause)*

I should like to thank the Government of Sweden for giving us—the Kenya Government—a grant of K.Sh. 19 million worth of fertilizer to help the small farmers who very much need it. For a long time they have been neglected but we have now come up. We have helped them but I still feel that they should be helped a lot more to produce food. Since we are in the process of re-organizing co-operative societies so that they do not cheat the co-operators, we hope that we will succeed in this venture. I also hope that those who are working, particularly the Commissioner of Co-operatives along with the Minister—

*(His Excellency the President looked around the Front Bench)*

**An hon. Member:** He was here! He has just gone out!

**His Excellency the President (Mr. arap Moi):** They should liaise with other people who are conversant with co-operative societies so that the co-operative societies have a deal, and so that they feel that they own the Co-operative Bank, they are share-holders and that they should take care of it. They should have a sense of "belonging"! Nobody should work as if he is a dictator; "I want this done; I want that done and so on". All of us, from me downwards, are servants of the people!

*(Applause)*

Although I would have liked to take a longer time, I merely wanted to say how pleased I am to note and to see hon. Members being very active in this particular Debate because it augurs well for the future, because the future depends on how much we produce ourselves. I hope we will continue to produce more and more. This year we have produced a lot of food and I am proud that we will have enough food given that no one will transport some of this food outside Kenya.

*(Applause)*

Our policy is to improve the lives of the people in the rural areas because although this Motion covers the National Food Policy, I believe that if we are determined to improve their ways of life genuinely, then every person, including district commissioners, district officers and so on, should make sure that the businessmen in the villages and all over the place are helped. And I may have to suggest that the district commissioners should be responsible in issuing trade licences



**[His Excellency the President]**

to wananchi in rural areas (villages) because trade officers tend to take people to villages when they should really remain around there. I do not want to expound on that one.

*(Applause)*

But I would like to see hon. Members seeing wananchi's problems, not only talking and paying them "lip service" as if you are the champions of their causes. Be champion of their causes in a humble way and help them. How many have you helped, physically?

*(Applause)*

I want hon. Members—if you allow me to talk—to do whatever they can, but as I have said let us live harmoniously. The philosophy of Nyayo which is "Peace, Love and Unity" does not accept hatred!

*(Applause)*

There are others who believe in character assassination and there are others who believe in witch-hunting. Why do you not build up your own wealth through proper means rather than hunt? So-and-so because you see him coming up and then hit him with a rungu? You then come out and blame Asians and Europeans and yet you do not want your own fellow Africans to come up. What you should be interested in is to get better genuinely. I want you to acquire wealth genuinely. I want you to acquire wealth genuinely and not through short-cuts.

*(Applause)*

That is the only way we can spread our wealth and see to the future and that is why I said that we must start from known to unknown. People tend to only look at what is known. For instance, in education where do you start from known things? Is it not in *thingira* where youngsters were being taught how to behave and how to grow up properly? the *thingira* of today is primary schools and that is why our youngsters get lost. They are not brought up properly. Their fathers come home late and find them asleep; the next morning they do not see them go off to school. They may even see them only once a week and even when they see them they are usually in a hurry and they tell them to go and see their mothers since they are busy. I think there should be a debate on this matter.

Mr. Deputy Speaker, I do not want to say things which may not be liked by hon. Members but I appeal to them all to be united and to serve this nation faithfully and devotedly, I myself, have given one of them responsibilities and they do not need to fight for positions. Let leadership come naturally just like a mother who

expects a baby in nine months should expect that baby right at that time. If she forces it to come out in six months or even five months, the baby may not be what was expected. So, we want to grow naturally as a nation. I hope some hon. Members will be able to find an opportunity to visit other countries and see for themselves what is happening there so that they can come home and see what we are doing in a better light. I am not saying that we are the best but I say that by African standards we are the best. But we need to do more; we need to be patriots; we need to love our country and we need to avoid tribalism at all costs.

*(Applause)*

Those youngsters at the University of Nairobi have nowhere else to go except to be integrated within our society and have jobs and do things for this country regardless of where they come from. I need your help in this matter and I ask you to preach this wherever you go so that our people can live in peace. The unity we have is just based on this, and the wananchi are happy. With these very few remarks, Mr. Deputy Speaker, I wholeheartedly support the Sessional Paper No. 4 of 1981.

#### POINT OF ORDER

##### *Early Adjournment of the House in honour of the President*

**The Minister for Local Government** (Mr. ole Oluotiipitip): I think hon. Members will realize that this is a very greater honour to us all. Now that our beloved President has concluded his speech. Would it not be in order for me to move that the House be now adjourned as a sign of respect to him? We could then leave those very good remarks for today and continue with the debate tomorrow.

*(Applause)*

**Hon. Members:** Put the question!

**Mr. Deputy Speaker:** Order! Well, I will leave it to the hon. House to decide on the matter.

*(Question, that the House be now adjourned, put and agreed to)*

#### ADJOURNMENT

**Mr. Deputy Speaker:** Hon. Members, the House is now adjourned until tomorrow, 2nd December, 1981, at 9 a.m.

*The House rose at ten minutes past Six o'clock.*

**Wednesday, 2nd December, 1981**

The House met at Nine o'clock.

[*Mr. Deputy Speaker in the Chair*]

PRAYERS

ORAL ANSWERS TO QUESTIONS

No. 333

FOREIGN FIRMS EMPLOYING NON-CITIZEN SECRETARIES

